# Misingi ya Agano la Kale: Mwongozo wa Kozi

**Pentatuku**
**Historia ya Zama za Kale**
**Baba Abrahamu**

## MAELEZO YA KOZI

Vitabu vya kwanza vitano vya Agano la Kale vinaitwa Pentatuku. Vinaeleza historia ya taifa la Israeli kuanzia uumbaji hadi maandalizi ya kuingia katika nchi ya ahadi. Lakini je, Pentatuku ni historia tu ya watu waliochaguliwa na Mungu, au kuna kitu cha ziada? Kozi hii inachunguza kitabu cha Mwanzo na kitabu cha Kutoka, ili kupata ukweli wa kwanini viliandikwa, vilikuwa na maana gani kwa wapokeaji wa awali, na jinsi gani tunaweza kuvitumia hivi leo.

Kozi hii imejengwa katika mfululizo wa mafundisho juu ya Pentatuku, Historia ya Zama za Kale, na Baba Abrahamu ambayo yameandaliwa na shirika la Huduma ya Milenia ya Tatu na kuongozwa na Dkt. Scott Redd na Dkt. Richard Pratt, Jr., na pia kuchangiwa na wanazuoni mbalimbali.

## MALENGO YA KOZI, MAKUSUDI NA ORODHA YA MODULI

### *Malengo*

Katika kozi hii, tunapenda kufikia malengo yafuatayo:

1. Tunatarajia kuwa utatumia vielelezo vyote vya kozi hii ili kujifunza kwanini vitabu vya Pentatuku viliandikwa, vilimaanisha nini kwa wapokeaji wa kwanza, na jinsi tunavyopaswa kuvipokea hivi leo.

2. Tunatarajia kuwa utakuwa katika imani yako, na kuwa utaendelea kutumaini neema ya Mungu na uongozi wake wa haki na upendo.

3. Tunatarajia kuwa utatumia mafundisho ya Pentatuku katika maisha yako, na kuendelea kuishi kwa imani.

### *Makusudi*

Kwa kufanya mambo yafuatayo, itakuwa ishara kuwa malengo haya yamefikiwa:

1. Kupata alama za kuridhisha katika mitihani, kudhihirisha kuwa unaweza kubaini taarifa muhimu kuhusu muundo, yaliyomo, maana halisi na matumizi ya sasa ya vitabu vya Pentatuku.

2. Kujibu maswali katika miongozo ya masomo, kuonesha jinsi ulivyotumia mafundisho ya kozi hii katika maisha yako, hasa ya kwamba unaishi kwa imani, kutumaini neema ya Mungu na uongozi wake wa haki na upendo.

**Orodha ya Moduli kwa Kozi ya Misingi ya Agano la Kale**

1. Utangulizi wa Pentatuku
2. Ulimwengu Uliokamilika
3. Paradiso Iliyopotea na Kupatikana
4. Ulimwengu Uliojaa Vurugu
5. Mwelekeo Sahihi
6. Maisha ya Abrahamu: Muundo, Yaliyomo, na Maana Halisi
7. Maisha ya Abrahamu: Matumizi ya Sasa
8. Yakobo, Mzee wa Ukoo
9. Yusufu na Ndugu Zake
10. Muhtasari wa Kitabu cha Kutoka

## MAELEZO KUHUSU VIPENGELE VYA KOZI

***Beji***

1. Kila juma katika mazungumzo yenu mtatenga muda kwaajili ya kufanyia kazi vipengele vya Beji. Mwongozo huu wenye kurasa mbili utampa mkufunzi wenu mwongozo wa jumla wa namna mnavyotakiwa kuendeleza ujuzi huu muhimu katika huduma.
2. Katika wiki chache za mwanzoni, tumia muda wako ukiwa na kikundi chako pamoja na mkufunzi wako kupitia mada za kujadili kwenye maelezo ya beji.
3. Baada ya kuweka msingi imara kupitia majadiliano ya kikundi, tumia wiki zilizobaki kuifanyia kazi beji (mambo ya kufanya).
4. Utapatiwa beji pale mkufunzi wako atakapojiridhisha kuwa umetimiza vigezo vya beji kwa mujibu wa maelekezo yake.

***Moduli***

1. Jifunze kwa kutazama video, kusikiliza sauti, au kusoma nukuu.
2. Kamilisha mwongozo wa kujifunza kwa kila somo. Miongozo ya kujifunza itakuandaa wewe kujibu maswali ya mitihani, mazoezi ya kwenye mitandao na kukusaidia kuyatumia mafundisho ya somo katika maisha yako binafsi.
3. Fanya mitihani ya kila somo, mitihani itatolewa na mkufunzi wako. Mitihani inaweza kurudiwa kama kuna ulazima, tunapendekeza ufikie alama zaidi ya asilimia 80% kabla ya kushiriki mjadala wa wiki na kuhakikisha kuwa umeelewa maneno kwa usahihi.
4. Shiriki katika majadiliano ya kila wiki kwenye kundi lako pamoja na mkufunzi wako, mkitumia miongozo kuhusu kozi na uwezo wa kutumia maneno kwa usahihi katika maisha yako au huduma yako. Tunapendekeza mijadala kupitia video isiwe chini ya saa limoja.

*Mtihani wa Mwisho*

Unaweza ukafanya majaribio zaidi ya mara moja kama ukihitaji kujipima, lakini unatakiwa ujifunze na kusubiri kwa muda wa saa moja kabla ya kufanya jaribio jingine. Alama yako rasmi itakuwa ile uliyofanya vizuri zaidi kwenye majaribio yako na tunapendekeza upate zaidi ya 80% kabla ya kuendelea na kozi inayofuata.

**ALAMA ZA UFAULU**

Daraja la mwisho la ufaulu litahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Majaribio ya darasani yatakuwa na alama 30 kila moja.
2. Mtihani wa mwisho utakuwa na alama 100.
3. Ripoti ya beji ya maombi haiwezi kubadilisha daraja lako lakini ni lazima ipitishwe na mkufunzi ili uwe umekamilisha kozi.

*Alama za jumla katika kozi zinazozidi 80% zinahesabiwa kuwa ni ufaulu.*

------------------------------------

## Walioshiriki Kuandaa kozi hii

**Dr. Steve Blakemore** ni profesa mwandamizi wa falsafa katika chuo kikuu cha Wesley Biblical Seminary.

**Dr. Stephen J. Bramer** ni mwenyekiti wa kitivo na profesa wa mafunzo ya tafasiri ya Biblia katika chuo kikuu maarufu cha Dallas Theological
Seminary.

**Dr. Robert B. Chisholm**, Jr. ni mwenyekiti wa kitivo na na profesa wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuuu maarufu cha Dallas Theological Seminary.

**Dr. Don Collett** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Trinity School for Ministry.

**Dr. Dorian Coover-Cox** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Dallas Theological Seminary.

**Dr. Brandon D. Crowe** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Agano Jipya katika chuo kikuu cha Westminster Theological Seminary.

**Prof. Thomas Egger** ni profesa msaidizi wa Theolojia ya ufafanuzi katika chuo kikuu cha Concordia Theological Seminary.

**Rev.Michael J. Glodo** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Biblia katika chuo kikuu cha Reformed Theological Seminary’s Orlando Campus.

**Dr. Douglas Gropp** ni profesa wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Redeemer Seminary in Dallas, Texas.

**Rev. Dr. Cyprian K. Guchienda** ni mchungaji kwa mataifa katika kanisa la Highlands Park Presbyterian Church in Dallas, Texas.

**Dr. Jim Hamilton** ni profesa mwandamizi wa theolojia ya Kibiblia katika chuo kikuu cha The Southern Baptist Theological Seminary and Preaching Pastor of Kenwood Baptist Church.

**Dr. Gordon H. Johnston** ni profesa wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Dallas Theological Seminary.

**Dr. Carol Kaminski** ni profesa wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Dr. Riad Kassis** ni mkurugengzi wa jimbo wa Overseas Council, huduma ya kimataifa ya kufundisha viongozi wa Kikristo

**Dr. Craig Keener** yeye ni mwenyekiti wa F.M. na Ada Thompson masomo ya Biblia katika chuo kikuu cha Asbury Theological Seminary.

**Dr. David Lamb** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Biblical Theological Seminary.

**Dr. Erika Moore** ni Profesa wa masomo ya Agano la kale na Kiebrania katika chuo kikuu cha Trinity School for Ministry.

**Dr. John Oswalt** ni ni profesa mwandamizi wa heshima wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Asbury Theological Seminary.

**Dr. Thomas Petter** ni profesa mwandamizi wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Dr. Richard L. Pratt, Jr.** ni Raisi wa huduma ya Third Millennium Ministries na ni profesa msaidizi wa masomo ya Agano la Kale katika chuo kikuu cha Reformed Theological Seminary's Orlando Campus.

**Rev. Dr. Paul R. Raabe** ni Profesa wa masomo ya Theolojia ya ufafanuzi katika chuo kikuu cha Concordia Seminary.

**Dr. J. Scott Redd** ni Raisi wa chuo kikuu cha Reformed Theological Seminary in Washington D.C. na pia ni profesa msaidizi wa masomo ya Agano la Kale.

**Dr. Brian D. Russell** ni Profesa wa masomo ya Biblia na kiongozi wa shule ya masomo ya huduma ya mijini katika chuo kikuu cha Asbury Theological Seminary's Orlando Campus.

**Dr. Timothy E. Saleska** ni mkuu wa kitivo cha matengenezo ya huduma na profesa mwandamizi wa theolojia ya ufafanuzi katika chuo kikuu cha Concordia Seminary.

**Dr. Douglas Stuart** ni Profesa wa masomo ya Agano la Kale na mwenyekiti wa masomo ya Biblia katika chuo kikuu cha Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Dr. David Talley** ni Profesa wa masomo ya Bilia na Theolojia katika chuo kikuu cha Talbot School of Theology.

**Rev. Dr. Michael Walker** ni mwanatheolojia mkazi katika kanisa la Highland Park Presbyterian Church in Dallas, Texas.

**Dr. Larry J. Waters** ni Profesa wa masomo ya Ufafanuzi wa Biblia katika chuo kikuu cha Dallas Theological Seminary.

**Dr. Michael D. Williams** ni Profesa wa masomo ya Theolojia ya Utaratibu katika chuo kikuu cha Covenant Theological Seminary.